**HOTUBA YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050, TAREHE 17 JULAI, 2025 - DODOMA**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!**

Niungane na walionitangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutukutanisha katika tukio hili la uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya **mwaka 2050.** Hili ni tukio la kihistoria, linaloweka msingi wa mustakabali wa Taifa letu kwa **miaka 25** ijayo, pamoja na mwelekeo mpya wa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa msingi huo, niwapongeze kwa dhati na kuwashukuru sana wale wote walioshiriki katika mchakato mzima wa kuandaa **Dira 2050**. Ninakumbuka wakati ninazindua mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Dira, nilielekeza kuwa mchakato huu uwe jumuishi kwa kadri iwezekanavyo ili maudhui yake yaweze kuakisi matakwa ya wananchi, kwenye dhana ya Tanzania Tunayoitaka. Hivyo, niwapongeze sana wananchi wote walioitikia wito wa kutoa maoni yao ili kuifanya Dira hii kuwa na umiliki wa kitaifa.

Nimefarijika kwamba ujumuishi wa mchakato wa Dira hii umeendelea hata katika uchapishaji wake, kwani leo hapa tutagawa nakala za **Dira 2050** ambazo zimeandikwa kwa mfumo wa nukta nundu ili ndugu zetu wenye changamoto za uoni waweze kuisoma pia. Hongereni sana kwa kuzingatia suala la wenye mahitaji maalum katika utayarishaji wa Dira hii.

Uandaaji wa Dira hii umehusisha watu wengi katika hatua mbali mbali. Imehusisha Wizara , Kamati ya Uongozi, Tume yenyewe, Sekretarieti, Kamati ya Wataalam na Wnaanchi kwa ujumla. Si rahisi kumtambua kila mmoja kwa jina lake, ila naomba niwataje baadhi:

***Kwanza***, nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Jakaya Kikwete, Rais Mstaafu na viongozi wote wastaafu kwa kushiriki kikamilifu kwenye mchakato na kwenye tukio hili hadi leo tunapoizindua Dira. Ninakushukuru Mhe. Rais Mstaafu kwa kuwasilisha hotuba kwa niaba ya wastaafu wa nchi yetu, lakini kubwa zaidi kwa kutupa ridhaa ya wastaafu ya kuendelea na utekelezaji wa Dira hii. Tunawashukuru sana.

Aidha, nimshukuru Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kutuzindulia mchakato huu wa Dira, na Rais wa Zanzibar Dkt. Mwinyi, kwa kutuzindulia rasimu ya Dira, na kwa ufuatiliaji wenu wa karibu wa zoezi hili. Mheshimiwa Dkt. Mpango ni gwiji wa mipango ya maendeleo katika nchi hii; alishiriki kuandaa Dira 2025, alishiriki kuandaa Programu ya *Big Results Now;* alikuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango iliyovunjwa na baadaye Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Fedha na Mipango. Tunathamini sana mchango wako Mheshimiwa Makamu wa Rais! Katika nafasi zote ulizofanyia kazi.

***Pili,*** niwashukuru Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Abdulla, kwa usimamizi wao thabiti kwa Kamati ya Uongozi ya Kitaifa ya Dira.

***Tatu***, Waziri wa Nchi Prof. Kitila Mkumbo, na Mawaziri Mwigulu Nchemba na Saada Mkuya,kwa utendaji wao na michango yao katika uandaaji wa Dira hii. Niishukuru Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kwa ujumla, na Tume ya Taifa ya Mipango, wakiongozwa na Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume kwa kujitolea kwao katika kufanya kazi hii ya kizalendo. Aidha, tunamkumbuka mtangulizi wa Dkt. Msemwa, Marehemu Lawrence Mafuru, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika mchakato wa maandalizi ya Dira. Mungu aendelee kuilaza roho yake mahala pema peponi.

***Nne***, Niwashukuru Makamishna wa Tume ya Taifa ya Mipango kwa mwongozo wao makini ulioiwezesha Tume kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi mkubwa.

***Tano,*** ninawashukuru pia kwa umuhimu wa kipekee, Timu Kuu ya Kitaalamu ya Dira 2050 iliyoongozwa awali na Prof. Lucian Msambichaka, na baadaye Balozi Dkt. Asha Rose Migiro kama Mwenyekiti wa Timu na Profesa Joseph Semboja, kama Makamu Mwenyekiti, pamoja na wataalam wenu wote. Mmelitendea haki Taifa letu na, Hongereni sana kwa kazi nzuri na ya kizalendo.

Kwa mnasaba wa shughuli hii, ninataka kuzungumzia masuala makubwa matano, yakijumuisha utajiri wa nchi yetu; mafunzo ya historia ya maendeleo; nafasi ya kila mmoja wetu katika kuifanikisha Dira; Tanzania tuitakayo kuelekea **2050**; na msisitizo kwenye kuitumikia nchi yetu kwa ufanisi zaidi.

## UTAJIRI WA NCHI YETU

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Ndugu Wananchi:***

Tanzania ni nchi iliyobarikiwa sana kwa utajiri wa maliasili, ardhi na jiografia au maumbile yake; na haya tumeyasema katika majukwaa mbalimbali. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliita Tanzania “lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika”, na majirani zetu wanasema *Tanzania is a land of plenty*. Lakini pia mtakubaliana nami kwamba, nchi hii tajiri bado ina watu wengi masikini. Kwa hivyo, changamoto yetu kubwa kama viongozi ni kubuni na kutekeleza mipango na mikakati madhubuti ya kuutumia utajiri wa nchi yetu katika kufaidisha maisha halisi ya Watanzania.

Tunayo mifano mingi ya nchi zilizokuwa masikini kwa rasilimali lakini watu wake wana ustawi mkubwa kutokana na mipango na mikakati waliyojiwekea. Hivyo, azma yetu ni kuhakikisha tunashusha faida zitokanazo na utajiri wa nchi yetu katika kuimarisha ustawi wa maisha ya wananchi wote.

***Ndugu Wananchi;***

Kichocheo kingine cha Utajiri wa nchi yetu ni kuwa na Taifa lenye umoja, mshikamano, amani na utulivu. Kuna msemo kwamba Mti wenye mizizi mirefu na madhubuti hautikiswi na dhoruba. Ndani ya kipindi cha miongo 6 ya Uhuru wa nchi yetu, dhoruba nyingi zimelitikisa bara la Afrika na kudhoofisha nchi nyingi. Ila Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizobakia imara. Tumeweza kudumisha utamaduni wa kidemokrasia wa kupokezana madaraka ya uongozi kwa njia ya amani. Mimi ni Rais wa Sita, nikitanguliwa na marais watano. Hii ni kwa sababu, historia ya Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejengeka katika Mizizi imara na madhubuti. Historia yetu imesimama katika misingi ya Umoja wa kitaifa, mshikamano na kuheshimiana, Utulivu wa kisiasa, Amani na usalama.

## MAENDELEO NI HATUA

***Ndugu Wananchi;***

Utulivu wa kisiasa,  Usalama na Amani nchini ndio kiini cha maendeleo wa Taifa lolote. ***Lakin maendeleo ni hatua.*** Tanzania ya miaka ya **1960** siyo Tanzania ya leo. Tukiangalia maendeleo ya kiuchumi, Serikali yetu imekuwa ikipiga hatua za maendeleo awamu baada ya awamu. Awamu ya kwanza ilitufundisha kuwa msingi wa taifa ni utu na usawa. Awamu ya pili ilitufungulia njia ya uchumi wa soko na demokrasia ya vyama vingi. Awamu ya tatu iliimarisha taasisi za uwajibikaji na utawala bora. Awamu ya nne iliongeza kasi ya maendeleo ya kijamii na huduma bora kwa wananchi, na ilikuwa na msemo 'Maisha bora kwa kila Mtanzania'. Msisitizo wa awamu ya tano ulikuwa ni kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na miradi mikubwa ya kimkakati.

Nami, pamoja na viongozi wenzangu katika Serikali, tumeendelea kujenga juu ya misingi iliyowekwa na watangulizi wetu. Serikali leo imejikita katika kuimarisha uchumi jumuishi na shindani, unaogusa maisha ya kila Mtanzania, kutoka mijini hadi vijijini. Tunaendelea na kazi ya kukuza uchumi, kuwezesha wanawake na vijana, kupanua wigo wa washiriki na wadau mbalimbali wa maendeleo na sekta binafsi, na kusukuma mbele mageuzi ya kisera na ya kijamii yatakayoleta mafanikio kwa wote. Kwa hivyo, mantiki ya kuandaa Dira za **miaka 25** ni kuhakikisha kunakuwa na uendelevu wa mipango na mikakati ya kuliendeleza Taifa.

Maendeleo ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii yanaonekana dhahiri kama ilivyoelezwa na Waziri wa Mipango na Uwekezaji na wasemaji wengine walionitangulia.

Pamoja na hayo, historia ya maendeleo ya Tanzania ina mafunzo ambayo tunapaswa kuyazingatia leo. Kuanzia Tamko la Azimio la Arusha hadi Dira ya mwaka 2000 hadi 2025. Hatukuweza kutimiza yote tuliyojipangia katika mipango yetu mbali mbali ya maendeleo kwa asilimia mia,  kutokana na mapungufu katika usimamizi na sheria, kuathiriwa na sera za kiuchumi za dunia, utegemezi wa kifedha, kiufundi na kiteknolojia, Majanga na mabadiliko ya tabia nchi.

Kutokana na uzoefu tulioupata katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya muda mrefu, tumedhamiria kuitekeleza **Dira 2050** kwa umakini mkubwa. Tutaweka umuhimu kwenye upangaji na usimamizi bora wa mipango ya maendeleo itakayoitafsiri dira hii, na tutaendelea kujenga uwezo wetu wa kifedha, kitaalamu na kiutendaji, na kujijengea uwezo wa kukabiliana na misukosuko ya kikanda na kimataifa.

***Pili***, misaada na mikopo inaweza kuchangia na kuwa sehemu lakini haiwezi kuwa msingi wa maendeleo endelevu, kwani wakati mwingine, inaambatana na masharti magumu yanayoathiri uhuru wetu wa kujiamulia mambo yetu kama Taifa. Hivyo, Kipaumbele chetu ni kulinda na kutumia rasilimali zilizomo nchini ziweze kujenga uchumi wa nchi na kuleta ustawi wa wananchi. Kwa ufupi, tunajenga msingi wa kuelekea kujitegemea. Tunajua ni safari ndefu na safari ngumu, lakini kwa uwezo wa Mungu tutafika.

## WAJIBU WA KILA MTANZANIA KATIKA UTEKELEZAJI WA DIRA 2050

***Ndugu Wananchi;***

Kama nilivyosema hapo awali, maudhui ya **Dira 2050** yametokana na maoni na matakwa ya Watanzania wenyewe. *Tumefikiri wenyewe; tumeandika wenyewe; tumepanga wenyewe; na tutatekeleza wenyewe,* kwa kushirikiana na wale tutakaoona wanatusaidia. Na kwa kuwa kila Mtanzania ni sehemu ya Dira hii, hatuna budi sote kushiriki katika utekelezaji wake

Dira 2050 imeweka bayana malengo na shabaha za maendeleo ili kuijenga Tanzania Tunayoitaka. Mheshimiwa Waziri ameyataja hapa, ikiwemo: kujenga uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani; Maisha bora na ustawi kwa wote; kujenga taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi; na kujenga jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wa nchi kimataifa. Na kwa kila lengo, zimebainishwa shabaha au malengo mahususi. Nataka kusema kuwa utekelezaji wa malengo haya pamoja na shabaha zake unahitaji jitihada za pamoja kati ya Serikali, sekta binafasi, mwananchi mmoja mmoja, na wadau wa maendeleo.

## TANZANIA TUITAKAYO KUELEKEA MWAKA 2050 KATIKA MAZINGIRA YA DUNIA YA SASA

***Ndugu Wananchi;***

Katika kuandaa **Dira 2050,** tumetafakari na kutathmini kwa kina historia yetu, na uzoefu wetu wa kutekeleza malengo na mikakati ya maendeleo tangu tupate Uhuru. Hivyo, tumeainisha kwa kina mafanikio yote katika utekelezaji wa **Dira 2025** pamoja na changamoto zake, na kuzingatia hali halisi ya dunia ya leo, ili hatimaye kuamua aina ya jamii tunayoitaka

na tunayoweza kuijenga kwa kuzingatia matarajio ya Watanzania. Baadhi ya masuala tuliyoyazingatia kutokana na hali halisi ya mazingira ya sasa ya dunia ni pamoja na haya yafuatayo:

***Kwanza***, ni mabadiliko ya mfumo na muundo wa uchumi wa dunia, ambao unaelekea kujikita zaidi katika uchumi wa maarifa, viwanda na huduma, na uongezaji wa thamani wa bidhaa. **Dira 2050** imelizingatia hili kikamilifu.

***Pili,*** Uchumi wa dunia unashuhudia mabadiliko makubwa kutoka kutawaliwa na Taifa moja lenye nguvu, kuelekea kuibuka kwa mataifa mengi yenye ushawishi kwenye maamuzi ya kiuchumi ngazi ya kimataifa. Hivyo, kutokana na mivutano ya mataifa hayo, Tanzania lazima tuendeleze sera yetu ya kutofungamana na upande wowote. Aidha, lazima tujipange kulinda maslahi yetu katika mazingira haya mapya ya kikanda na kimataifa. Suala hili pia limezingatiwa kikamilifu katika Dira hii ya 2050.

***Tatu***, mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabia nchi yanaendelea kuathiri sera za kitaifa na kimataifa, ikiwemo suala la uzalishaji na usalama wa chakula. Tanzania lazima tuendelee kujipambanua na kuwa sehemu ya juhudi za kimataifa za kulinda mazingira, na vilevile kuweka mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi nchini mwetu. Hili nalo limezingatiwa kikamilifu katia **Dira 2050**.

***Nne***, mabadiliko ya kidemografia duniani. Wakati nchi mbalimbali zilizoendelea zinashuhudia ongezeko la idadi ya wazee, barani Afrika, kuna ongezeko kubwa la vijana. Katika nchi yetu, zaidi ya **asilimia 76** ya idadi ya watu wapo chini ya **miaka 36**. Hii inamaanisha kuwa, tuna mtaji mkubwa wa nguvukazi ya kusukuma maendeleo. Inatulazimu tuendelee kuwekeza sana katika sekta za Ustawi wa jamii ili kulinda nguvu kazi ya Taifa. Aidha, lazima pia tuwe makini na mapokeo ya teknolojia za kisasa ili kulinda ajira za watu wetu. Haya nayo yamezingatiwa kikamilifu katika **Dira 2050.** Niseme kuwa nimefurahishwa na mwelekeo wa sekta binafsi nchini na Serikali inakarabisha mapendekezo ya sekta binafsi kama yalivyowasilishwa na mwakilishi wao.

***Tano,*** mapinduzi makubwa ya kiteknolojia na maendeleo ya kidijitali. Dunia inashuhudia maendeleo makubwa na ya haraka katika akili unde (AI) na teknolojia nyingine. Lazima, tujipange na tuwe sehemu ya kutumia, kusababisha na kumiliki mabadiliko haya. Hili nalo limezingatiwa kikamilifu katika **Dira mpya.**

Kwa ufupi, ***Ndugu Wananchi***, **Dira 2050** imezingatia kikamilifu muktadha wa dunia ya leo iliyojaa mabadiliko makubwa na changamoto zisizotabirika, Ila vile vile ni dunia yenye fursa nyingi. Kufuatia tathmini hiyo tumejiwekea lengo la kujenga ***Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea.*** Na hiyo ndiyo Tanzania tunayoitaka katika **miaka 25** ijayo!

## SASA TWENDENI KWENYE VITENDO

***Ndugu Wananchi;***

Tunapozindua **Dira 2050** tujielekeze katika vitendo zaidi kuliko maneno. Wazee wetu walisema *lisilo budi hutendwa*, hawakusema *lisilo budi husemwa*. Sasa sote, Serikali, sekta binafsi na wananchi, tutende zaidi kuliko kusema. Hii ina maana kwamba mtihani halisi wa Dira hii utakuwa kwenye utekelezaji wake. Ni lazima tufikiri, tupange na tutende kimkakati.

Misingi tuliyofundishwa ni kwamba “Kupanga ni kuchagua.” Kwa kuzingatia dhana hiyo, **Dira 2050** imebainisha vigezo mahsusi vitano vya kuchagua sekta za vipaumbele. Vigezo hivi ni *uwezo wa kuzalisha ajira kwa wingi; uwezo wa kuongeza mauzo ya nje; uwezo wa kuchochea ukuaji wa sekta nyingine; uwezo wa kuongeza thamani hapa nchini; na uwezo wa kukuza mapato ya Serikali.* Kwa msingi wa vigezo hivi, **Dira 2050** imechagua sekta za kimageuzi tisa kwa hatua ya sasa. Sekta hizi ni: *kilimo, utalii, viwanda, ujenzi, madini, uchumi wa buluu, michezo na ubunifu, huduma za kifedha, na sekta ya huduma.* Nataka nisisitize tena, pamoja na vigezo hivi, thamani ya kweli ya Dira 2050 itapimwa kwa uwezo wetu wa kuitafsiri kwa vitendo, katika mipango, bajeti na maamuzi mbalimbali. Kwa hivyo, hatuna budi kuzingatia suala la uwajibikaji wa pamoja.

## HITIMISHO: TUAMSHE KIU NA VUGUVUGU LA KUSAKA MAENDELEO

***Ndugu Wananchi;***

Ni matumaini yangu kuwa uzinduzi wa Dira 2050 utaamsha ari ya kila mwananchi kwa nafasi yake kuchangia katika kutosheleza kiu ya Tanzania ya maendeleo endelevu, au Tanzania Tuitakayo.

Mtakubaliana nami kwamba, kuna hali ya kudorora kwa ari ya kujadili masuala ya maendeleo katika jamii yetu, hususan miongoni mwa vijana ambao ndio tegemeo letu katika kujenga kesho iliyo bora. Hii sio sawa hata kidogo. Katika **miaka 25** ijayo, lazima turudishe

mijadala ya maendeleo katika nchi yetu. Mipango ijadiliwe na vijana na wajipange nvyema kama ilivyokuwa misingi yetu ya awali.

***Ndugu Wananchi***, ninapohitimisha napenda kutoa wito na maelekezo yafuatayo:

***Kwanza***, tubadili mtazamo na namna tunavyofanya kazi na kupimana, kwani Dira 2050 imeweka lengo na shabaha kubwa - kufika uchumi wa kati wa juu, wa **dola trilioni moja**. Ni wazi kuwa hatutoweza kulifikia lengo hilo kama tutaendelea kufanya kazi kwa mazoea. Lazima tubadilike kifikra, kimtazamo na kimatendo. Vilevile, lazima tupimane kwa matokeo ya kazi.

Hivyo, ninaelekeza Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa haraka na kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa **Dira 2050** nyenzo zitakazotumika kupima matokeo ya utendaji Serikalini kwa kuzingatia malengo na shabaha za **Dira 2050**.

***Pili***, kila Wizara ipitie sera zake na kuhakikisha zinashabihiana na maudhui ya **Dira 2050**. Sera ambazo haziendani na maudhui hayo hazina budi kufanyiwa mapitio na kurekebishwa ***kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa Dira 2050 hapo Julai 1, 2026***. Sekretarieti ya Tume ya Taifa ya Mipango iratibu zoezi hili.

Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali nao vilevile waanze mchakato wa kuchambua na kuja na mapendekezo ya maboresho ya kisheria ili kuwezesha utekelezaji kamili wa Dira hii.

***Tatu,*** ninaelekeza Tume ya Taifa ya Mipango pia kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Mfumo huu lazima uwe wa kitaasisi, unaoweka wazi majukumu, muda wa utekelezaji, na njia ya kupima mafanikio kwa kila hatua. Uratibu wa utekelezaji uzingatie mshikamano wa ngazi zote za Serikali, kuanzia Serikali Kuu hadi Serikali za Mitaa, pamoja na ushirikiano wa karibu kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, jamii na wadau wa maendeleo. Kila taasisi ya Serikali italazimika kuwa na vigezo vya kupima utendaji *(Key Performance Indicators-KPIs)* vinavyoendana na malengo na shabaha ya Dira.

Aidha, utekelezaji huu lazima uendeshwe kwa uwazi. Taarifa za maendeleo ziwe wazi na zipatikane kwa umma ili kujenga uaminifu, na kuhimiza ushiriki wa wananchi katika safari ya kujenga Tanzania Tunayoitaka.

***Nne,*** sekta binafsi ndio mhimili wa ujenzi wa uchumi wetu, hakuna shaka na hilo. Sekta hii nayo ijipange vyema katika kutekeleza malengo, shabaha za **Dira 2050**. Utekelezaji wa **Dira 2050** unahitaji ushiriki wa dhati na wa kimkakati kutoka kwa sekta binafsi katika maeneo yote ya Uchumi: uwekezaji, ubunifu, uundaji wa ajira zenye staha, na uboreshaji wa tija katika kila sekta. Ahadi yetu kwenu ni kuwa Serikali itazingatia mapendekezo yote mliyotuletea na tutayafanyia kazi kwa pamoja nanyi,

***Tano*****,** katika kuhakikisha ushirikishwaji kwenye utekelezaji wa Dira 2050, wekeni mkakati wa mawasiliano, elimu kwa umma na uhamasishaji kuhusu Dira ili watendaji wetu, wananchi na wadau wetu waelewe nafasi na mchango wao kuelekea **2050**.

***Sita,*** Dira imeweka msisitizo wa kipekee katika suala la haki, na vilevile katika kulinda maadili na utamaduni wa Tanzania. Haya ni maeneo muhimu sana kwa ustawi wetu kama Tanzania. Hapa nitoe wito kwa Mahakama ya Tanzania na taasisi zote husika katika utoaji haki kutambua nafasi yao katika kufanikisha malengo ya Dira, na kutimiza wajibu wao bila upendeleo, ghuba wala chuku au uonevu kwa mtu yeyote.

Vilevile, nitoe rai kwa taasisi za kijamii, zikiwemo taasisi za kidini, ambazo zimekuwa mhimili katika kujenga jamii yenye maadili, na kusimamia kidete ujenzi wa Tanzania Tunayoitaka yenye maadili.

## MWISHO

***Ndugu Wananchi,***

Kila jambo linakuwa na wadadisi. Sasa kuna wadadisi ambao wanaweza kuuliza kwa nini kama Taifa tumejiwekea lengo kubwa na shabaha kubwa ya maendeleo yetu na vizazi vyetu. Jibu letu ni moja: kwa ukubwa wa rasilimali, ari na uwezo wa Watanzania, hatuna sababu yeyote ya kutoweka lengo kubwa kwa kesho yetu na ustawi wa Taifa letu. Tumeweza

kutekeleza mengi. Tutaweza kuitekeleza Dira hii. Kwa hiyo Watanzania tujipe moyo, tukae tayari, na tuwe tayari kuchangia ili Dira hii itekelezwe vizuri.

***Ndugu Wananchi,***

Nilianza hotuba yangu kwa kuainisha sifa na utajiri wa Taifa letu. Sasa tukitumia sifa hizo na utajiri huo kwa maarifa na bidii tutafanikiwa, tutapiga hatua zaidi za maendeleo, na tutafikia malengo ya Dira 2050. Kwa pamoja, tushirikiane na tutimize wajibu wetu katika kulijenga ***Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea.***

**Baada ya kusema hayo, pamoja na shukrani nyingi, sasa, ni heshima yangu kutamka kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imezinduliwa rasmi!**

***Mungu Ibariki Afrika!***

***Mungu Ibariki Tanzania!***

***Mungu Ibariki Dira 2050!***

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!***